
# Siku nilipokuita, ulinisikiliza ee Bwana

*Zaburi 137, 1-2a,2bc-3,6-7ab,7c-8*

*Siku ya Mungu ya 17 Mwaka C* — *Rodriguez NTUGULO*




1. *Nitakutukuza, ee Bwana, kwa moyo wangu wote,*
   *kwani umesikia maneno ya kinywa changu.*
   *Mbele ya malaika nitakuimbia,*
   *nitaliangukia hekalu lako takatifu.*
2. *Nitatukuza jina lako, kwa ajili ya wema wa uaminifu wako.*
   *Kwa maana umekuza kuliko yote jina lako na ahadi yako.*
   *Siku nilipokuita ulinisikiliza,*
   *uliongeza nguvu rohoni mwangu.*
3. *Bwana yuko juu, lakini anamwangalia mnyonge,*
   *na mwenye kiburi anamtambua toka mbali.*
   *Ninapo kwenda katiya taabu, Wewe unasitawisha uzima wangu.*
   *unanyosha mkono wako kuizuia hasira ya adui zangu.*
4. *Mkono wako wakuume unanisalimisha;*
   *Bwana atatimiliza kwangu aliyonitendea.*
   *Ee Bwana, wema wako ndio wa milele:*
   *usiache kazi ya mikono yako.*